



Transcript: Kuuliza si ujinga.

- Kuluthumu: Asante, sana kwa kuja maana mama Rukia aliniambia utakuja leo. Sasa ngoja mimi nikuachie niende kazini kwangu maana kuna shughuli huko, nitakuacha hapa utwange hizi karanga si unajua kufua na kufanya kazi zote?
- Amina: Ndiyo, mama najua!
- Kuluthumu: Basi, utapika wali na maharage siunajua kutumia nazi?
- Amina: Ndiyo, mama najua kutumia.
- Kuluthumu: Mbuzi ya kukuna nazi ipo jikoni, kila kitu kipo hapo jikoni.
- Amina: Asante mama kwa kazi.
- Kuluthumu: Karibu sana, sasa endelea kutwanga hizi karanga ngoja mimi niende kazini, watoto wakitoka shuleni utawaambia wakusaidie kufagia hapa.
- Amina: Sawa, mama.
- Amina: Ngoja nikapike chakula aliniambia, mbuzi yupo pembeni mwa jiko na mimi sioni mbuzi yoyote mimi nitapika hivyo hivyo...
- Kuluthumu: Hodi hapa?
- Amina: Karibu mama.
- Kuluthumu: Asante, za kushinda?
- Amina: Nzuri tuu mama.
- Kuluthumu: Sijui chakula kipo tayari maana nina njaa.
- Amina: Kipo tayari mama.
- Kuluthumu: Watoto wametoka shule?

Amina: Ndiyo mama.

Watoto: Shikamoo mama!

Kuluthumu: Marahaba habari za shule?

Watoto: Nzuri mama.

Kuluthumu: Amina, andaa chakula tule.

Amina: Sawa, mama.

Amina: Karibu, mama chakula.

Kuluthumu: Hahaaa! Ndiyo umefanya nini sasa Amina?

Amina: Nisamehe mamaangu sikujua!

Watoto: Mama, hiki ndiyo chakula gani?

Kuluthumu: Amina ulikosa mbuzi?

Amina: Nilimtafuta mbuzi huku nje lakini sikumuona.

Kuluthumu: Namaanisha mbuzi kibao cha kukunia nazi, nazi haipikwi hivi, nazi inakunwa, kama ulikuwa hujui si ungeuliza?

Amina: Nisamehe mama yangu sikujua.

Kuluthumu: Haya chukua hichi chakula peleka jikoni siku nyingine usirudie uwe unauliza, kuuliza si ujinga.

Vocabulary

- Kutangwa - To pound/ grind

- Mbuzi - goat/ a tool to scrape coconut